


# “MAHUSIANO YETU TANO (5) NA MUNGU"

Hujambo! Natumai hujambo asubuhi ya leo.

Wiki iliyopita tulitizama nia Kuu ya Mungu - kile ambacho Mungu anakifanya ulimwenguni. Tulijifunza kwamba anajitengenezea Watu wa kipekee - Watu wanaoitwa kwa Jina lake - Watu wanaotambua na kuutafakari utukufu wake - Watu ambao anakuja kukaa ndani yao sasa na milele.

Kwa kusudi hilo, Mungu alituumba kwa mfano wake mwenyewe, ili tuweze kuwa na uhusiano pamoja naye.

Kwa miaka mingi nimefikiria sana kuhusu maana ya kuwa na uhusiano na Mungu. Nina hakika kuna njia nyingi za kuelewa vipengele vingi vya uhusiano naye.

Ninajaribu kueleza kuelewa kwangu katika fundisho hili rahisi nitakaloliita “Mahusiano Yetu 5 na Mungu.”

Natumai ‘kifurushi' hiki kidogo kitakusaidia kuelewa vyema uhusiano wako na Mungu – na labda kukusaidia kuwasaidia wengine kuingia katika uhusiano kamili naye.

Leo nitayatambulisha kwa ufupi Mahusiano hayo matano - kisha wiki chache zijazo tutajadili kila moja kwa undani zaidi:

• UHUSIANO WA KWANZA;
Uhusiano wetu wa KWANZA na Mungu ni uhusiano kati ya VIUMBE WA KIPEKEE (sisi) na MUUMBAJI (Mungu). Mungu alituumba sisi. Sisi ni sehemu kubwa zaidi katika uumbaji wake. Sisi ni wa kipekee - tumeumbwa tuwe na uwezo wa kumjua Mungu, kuwa na uhusiano naye. Tunaanza muungano huu kwa kukiri; “Kuna mambo mawili ninayoyajua: “Kuna MUNGU. Mimi sio yeye!”

• UHUSIANO WA PILI;
Uhusiano wetu wa PILI na Mungu ni Uhusiano kati ya MTUMISHI na BWANA WAKE. Hatuishi kwa kujitegemea. Tunaishi kutoka kwa kuutegemea ukuu wa Mungu. Tunaishi chini ya mamlaka yake. Anatujali kwa uaminifu kama Watu wake. Tunatumika kama watumishi kwa uaminifu na radhi ya Mfalme na Bwana wetu (Mungu).

• UHUSIANO WA TATU;
Uhusiano wetu wa TATU na Mungu ni uhusiano kati ya RAFIKI na RAFIKI. Mojawapo ya mambo ya kushangaza zaidi kumhusu Mungu ni kwamba anataka kuwa rafiki yetu. Anataka tujuane - tuaminiane - tukae pamoja - tufanye mambo pamoja - tushiriki pamoja kwa uhuru - tuwe wepesi wa hasira na wepesi wa kusamehe.

• UHUSIANO WA NNE;
Uhusiano wetu wa NNE na Mungu ni uhusiano kati ya MTOTO na BABA YAKE. Marafiki ni wazuri. Lakini urafiki unaweza kuja na kwenda. Familia ndiyo hubaki. Mungu anataka tuwe zaidi ya watumishi - anataka tuwe watoto wake - familia yake. Mungu anawapenda watoto wake. Na sisi watoto wake tunampenda pia.

• UHUSIANO WA TANO;
Hatimaye, Uhusiano wetu wa TANO na Mungu ni ule wa MCHEZAJI na KOCHA. Tumeumbwa kama viumbe - watumishi - marafiki - na wana waliochaguliwa kuwa wachezaji hai kwenye Timu ya Mungu.

Sisi ni wachezaji wa Timu ya Yesu iliyojitolea kulikamilisha nia kuu ya Mungu. Mungu ndiye mkufunzi wetu. Roho wake Mtakatifu huwafunza na kuwaongoza Watu wake - Timu yake. Yeye ndiye kocha wetu anayetuongoza kwenye Ubingwa wa zama na Zama!

Mahusiano haya matano ni ya kiutendaji. Yana nguvu. Yameunganishwa. Ni mahusiano muhimu. Mahusiano haya yanatambulisha uhusiano wangu binafsi na Mungu. Yanatutia alama, pamoja na kututambulisha kwa wengine kama Watu wa Mungu.

Ni katika Kristo Yesu pekee ndio tunaweza kufanikiwa katika Mahusiano haya matano na Mungu. Watu wake pekee - ambao ni viumbe wake - waja wake - marafiki zake - watoto wake - na wachezaji wenzake - ndio wanaweza kuishi hivi.

Habari Njema ni kwamba Mungu anamwalika kila mtu ulimwenguni kuwa katika Mahusiano haya matano Naye.

Ndiyo maana tunashuhudia. Ndiyo maana tunahubiri. Ndiyo maana tunawaombea wagonjwa. Ndiyo maana tunatoa pepo. Ndiyo maana tunasamehe. Ndio maana tunawapenda wasiopendeza au kupendeka. Yote haya ni kuwaonyesha wengine kuwa pia wanaweza kuingia katika Mahusiano haya matano na Mungu. Ili waweze kumjua Mungu wa Biblia kama Muumba - Bwana - Rafiki - Baba - na Kocha.

Wiki tano zijazo tutajadili mahusiano haya tano na Mungu kwa undani. Ninaomba kwamba utaweza kupata ukomavu kamili katika Kristo Yesu unapokuza kila uhusiano kwa ukamilifu.

Ubarikiwe sana katika jina la Yesu.

Ni wako

*Douglas*

Douglas Van Devender.

Huduma za 'Jesus Ministries International' na 'Transforming Prayer'.

**TANGAZO LA KUZINGATIA:**
Wengine wanaweza kuongezwa kwenye orodha yetu ya barua-pepe kwa kutuma majina yao, eneo na barua pepe kwa WDV2023@outlook.com
(Mtu yeyote anaweza kujiondoa kwa kutuma neno STOP kwa anwani sawa ya barua pepe.) Ahsante.